**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

**SHULE YA SEKONDARI MAKIBA**

**S. L. P 13818**

**ARUSHA**

**TAREHE ………………………….**

**Namba za simu**

Mkuu wa Shule: **0658279170/0754279170**

Makamu Mkuu wa Shule: **0768075981/0676875981**

**KUMB. NA. MSS/K5/2023**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………………

S.L.P …………………

……………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKIBA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA MERU MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024 Tahasusi ya (i) CBG……….. (ii) HGL…..... Shule ya sekondari Makiba ipo kitongoji cha Korona, kijiji cha Makiba, kata ya Makiba, tarafa ya Mbuguni, halmashauri ya wilaya ya Meru, Kusini-Mashariki mwa Jiji la Arusha. Unaweza kufika shule ya sekondari Makiba kupitia Arusha Mjini-Kikatiti (Kilometa 32) kisha Kikatiti Makiba (Kilometa 21) . Pia waweza kufika shuleni kupitia Arusha-Tengeru-Mbuguni-Mirerani-Makiba ama Arusha-Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) Stand (Kilometa 45) kisha KIA Stand- Mirerani

(Kilometa 30) kisha Mirerani-Makiba (Kilometa 4.5).Kutoka Manispaa ya Moshi-KIA Stand (Kilometa 35) kisha KIA Stand - Makiba (Kilometa 34.5).

- Kwa wale ambao wanatokea mikoa ya kanda ya ziwa kupitia Babati watashukia kituo Kikuu cha mabasi Arusha Mjini kisha kupanda gari mpaka Mirerani ni shilingi 4,000/= na kisha kuchukua pikipiki kutoka Mirerani hadi Makiba kwa shilingi 3,000/=
- Kama utakosa gari la moja kwa moja kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha Mjini hadi Mirerani unaweza ukapanda gari kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha hadi Kikatiti kwa shilingi 1,500/= kisha ukapanda pikipiki hadi Makiba kwa shilingi 5,000/= ama waweza kupanda gari kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha hadi Standi ya KIA kwa shilingi 2000/= kisha upande daladala hadi Mirerani kwa shilingi 1,500/= kisha ukapanda pikipiki kwa shilingi 3,000/=
- Kwa wale wanaotokea mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro kwa kupitia Moshi, watashukia kituo cha KIA kisha kupanda daladala kwenda Mirerani kwa shilingi 1500/= kisha watashukia kituo kinachoitwa Getini-Mirerani kisha kupanda daladala hadi Makiba kwa shilingi 3,000/=

Unaweza kuwasiliana kwa namba za simu hapo juu kwa maelezo zaidi.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **…………** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………………**kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………………..**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:-**

**2.1 SARE YA SHULE (SCHOOL UNIFORM)**

**a)** Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mirefu yasiyo na maridadi yasiyoonesha ndani (non transparent) na sio kubana mwili.
**b)** Suruari mbili (2) rangi ya **BLUE BAHARI** yenye marinda mbili (2) na zisizobana mwili.
**c)** Sweta rangi **BLUE BAHARI.**
**d)** Tai rangi **NYEUSI** yenye michirizi myeupe iwe ndefu kiasi.
**e)** Sare za michezo ni rangi **BLUE** (Tisheti, kaptula na soksi)
**f)** Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi visivyo na urembo, vinapakwa rangi, viatu vyenye visigino virefu, visivyo na soli, ama vya plastic havitaruhusiwa.Atakaye kiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.
**g)** Soksi nyeusi jozi mbili
**h)** Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali na usio na balkon kubwa isiyokuwa na picha yoyote.
**i)** Nguo za kushindia (shamba dress) T shet ya kijani shingo ya duara isiyo na maandishi yoyote na suruali ya rangi nyeusi.
**j)** Tshet Dark Bluu ya Kola (Unaweza kuipata Jirani na shuleni).
**k)** **2.2** michango.

**a)** Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi:-

| Na | Aina ya michango | kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| 5. | Jumla | **80,000/=** |

**c)** MAHITAJI YA LAZIMA UNAYOTAKIWA KULETA

**i.** Ream 2 kwa mwaka yaani **Pain paper** 1( isiyo na mistari) na **Ruled paper** 1 (iliyo na mistari).

**ii.** Vitabu vya masomo hivi ni kwa ajili kumsaidia mwanafunzi kwenye masomo yake ya binafsi

- **General Studies:**
  - Understanding General Studies Advanced Level by Biligwamungu.
- **Chemistry:**
  - **GENERAL CHEMISTRY**
  - **PHYSICAL CHEMISTRY**
  - **ORGANIC CHEMISTRY**
  - **INORGANIC CHEMISTRY**
  - **Chemistry by Chande**
- **Biology:**
  - **BIOLOGICAL SCIENCE**
  - **Understanding Biology for A level by Susan Toole & G. Tool**
  - **Biology: A functional approach by B.M. V Roberts.**
- **Geography:**
  - **A comprehensive Approach to Physical Geography – D.T. Msabila.**
  - **Practical geography by Zisti Kamili.**
  - **Integrated approach.**
- **History:**
  - **Essentials in Advanced Levels History paper 1 + paper 2 by Saleh Yassin.**
  - **History 1 + 2 by Bakari Madaya.**
  - **Contemporary History Events by Shibitali C.K Tumaini.**
- **English Language I**
  - **Advanced Level English by Asheri, N.**
  - **Adavanced English Language by Oxford.**
- **English Language II**
  - **English Language for secondary school, Literature & stylistics for form v & vi.**
  - **Advanced Level Literature by Asheri, N.**

- **Poetry**

- **Selected Poems by TIE.**
- **The wonderful surgeon and other poems by Charles Mloka.**

➢ **Novels and short stories (aje na vitabu viwili kati ya hivyo)**
- **The Beautiful Ones Are Not Yet Born by Ayi Kwei Armah.**
- **A Man of the People by Chinua Achebe.**
- **Divine Providence by Severin N. Ndunguru.**
- **His Excellence Head of State by Danny Safo.**
- **Encounters from Africa by Macmillan Eduaction Limited.**

➢ **Plays (aje na vitabu viwili kati ya hivi)**
- **Betrayal in the City by Francis Imbunga.**
- **I Will Marry When I want by Ngugi wa Thiong'o**
- **Lwanda Magere by Okoiti Omtatah.**
- **An Enemy of the People by John Ruganda.**

**iii.** Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology.

**iv.** Sccientific calculator.

**v.** Laboratory coat kwa wanafunzi wa CBG.

**vi.** Mathematical set, kalamu za wino (bluu/nyeusi ball pens za kutosha), penseli na vifaa vingine vya kujifunzia

**vii.** Madaftari (counter books ya kutosha masomo 10.

**viii.** Majalada (File cover) mawili ya plastiki kwa ajili ya kufungulia faili na kutunzia mitihani na majaribio.

**ix.** Picha za Passport size 2.

**x.** Kamusi kubwa ya kiingereza (Dictionery) kati ya Oxford au Cambridge

**xi.** Begi au mfuko mzuri wa kuwekea vifaa vya shule.

**xii.** Sanduku imara la kuhifadhia mali yako.Tutapokea sanduku moja tu la **'TRANKA'**

**xiii.** Mahitaji yote ya bafuni mafano sabuni, mafuta, msawaki, taulo nk.

**xiv.** Godoro futi 3 kwa 6.

**xv.** Mashuka pair 2, foronya 1 (vyote hivi rangi ya bluu bahari), blanketi 1 na chandarua 1 rangi yoyote vyote viwili.

**xvi.** Vyombo vya chakula(sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

**xvii.** Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko

**xviii.** Kwanja 1, jembe 1, hard bloom, fagio (chelewa), mopa na skuiza kwa ajili ya usafi.

**xix.** Ulete result slip nakala halisi pamoja na nakala kivuli moja (original and copy) shuleni.

Kaulimbiu ya shule yetu ni: **MBELE DAIMA NYUMA MWIKO**

Lengo letu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri na hivyo kumuwezesha kufanikisha lengo la alichokifuata hapa.Sheria hzi zitasaidia kuleta hali ya AMANI, UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia bora. Kila mwanafunzi aje a nia ya KUSOMA KWA BIDII na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya MAKIBA SEKONDARI.

Kwa upande wa shule, sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU tutajitahidi kuishi, kumfundisha na kumlea mtoto lakini tutashindwa katika kazi hii bila ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi.

Vifuatavyo ni vifungu muhimu vya sharia za shule.Kila mwanafunzi anapaswa kuzizifuata sheria hizi kikamilifu.

- Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni kiingereza tu.Hii itasaidia kuleta ufanisi katika masomo.
- Kwa vile shuleni ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na ukimya hasa sehemu za madarasani
- Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama ratiba kuu ya shule inavyoonesha.
- Kazi za mikono ni moja ya elimu inayotolewa hapa shuleni hivyo kila mwanafunzi hana budi kushiriki kikamilifu bila kutegea.
- Hairuhusiwi kupeleka chakula nje ya bwalo la chakula kama bwenini.Wagonjwa watapelekewa chakula kwa kufuata taratibu zilizowekwa
- Mwanafunzi haruhusiwi kuleta chakula cha aina yoyote pindi arudipo shuleni toka likizo au arejeapo baada ya kupata kibali kutoka ndani ya shule.
- Mavazi yote ya binafsi hayahitajiki shuleni.Mwanafunzi atalazimika kuvaa sare na nguo za kushindia tu (shamba dress) isipokuwa muda wa michezo ambapo atavaa sare za michezo.
- Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote bwenini.Kwa mwanafunzi mwenye dawa atoe taarifa kwa Patroni ili ziweze kuhifadhiwa.
- Wanafunzi hawaruhusiwi kupeana dawa bwenini.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vyombo vya muziki kama vile redio,Walkman, earphone na headphone , kamera n.k
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu, kuhifadhi simu.
- Wizi, matusi na ugomvi haviruhusiwi kabisa
- Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki silaha ama kuwa na vitu vya hatari vya ncha kali kama vile visu, nondo, rungu, n.k
- Kila mmoja anawajibika kuvitunza vifaa vyote vya shule vya shule atakavyo kabidhiwa na alivyokabidhi kwa uangalifu wa hali ya juu vifaa vyote vya shule atakavyokabidhiwa na asivyokabidhiwa.
- Uharibifu au upotevu wowote utakaotokea, gharama za matengenezo au fidia zitalipwa na atakayefanya uharibifu huo.
- Kila IJUMAA, JUMAMOSI na JUMAPILI wale waendao kusali kwenye madhehebu mbalimbali watavaa sare za shule na kurudi baada ya sala zao kukamilika
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu watu wote hapa shuleni pamoja na uongozi wa shule na uongozi wa wananafunzi atumie lugha safi kwa watu watu wote na atatoa matatizo yake kwa viongozi wake kwa kufuata utaratibu husika.
- Ni marufuku mwanafunzi kwenda nje ya shule ama kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi wa shule bila kibali.
- Mwanafunzi ataenda kununua mahitaji kwenye duka la shule mudawa mapumziko tu.

3.**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu ama mtu yeyote yule
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi ama unywaji wa pombe na mwatumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati. Uhusiano wa jinsi moja, kuoa
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi
xi. Kusababisha mimba/ujauzito ama kumpa mimba msichana
xii. Kutembelea nyumba za starehe ama nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa ama kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kamaa kunywa sumu nk
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

4.**Viambatanisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Michoro ya muonekano wa mavazi/sare za shule jinsi zitakavyoshonwa.
e) Picha nne za passport size za mwanafunzi.

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**MUHIMU.**

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu kwa namna yoyote ile ,na hakuna mtumishi anayerusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………….**
**Jina la Mkuu wa Shule……………………………….**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………….**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII**

Mimi………………………………………………………………………. ( jina kamili)

Kidato cha……………………………………………… mwaka ……………………

Nakubali na naahidi kufuata sheria na taratibu za shule kama zilivyopangwa . Nikienda kinyume nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Tarehe ……………………………… …………………………….

Jina na sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe ……………………………... ………………………………….

Sahihi ya Mkuu wa Shule

Mimi Mzazi/ Mlezi wa ………………………………… nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheri na kanuni za shule . Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo

Tarehe ……………………………… Jina na sahihi ya Mzazi/ Mlezi……………………………

Tarehe ………………………………. Jina na sahihi ya shahidi………………………………….

Tarehe ……………………………. Sahihi ya Mkuu wa shule ……………………………………

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MAKIBA SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Makiba Secondary School.

Full name ------------------------------------------------------------------------------------------

Age: ---------------------------------------------------------------------------------------------------

1. “AIDS’ Test ---------------------------------------------------------------------------------

2. Blood count (red & white) ---------------------------------------------------------------

3. Urine examination ----------------------------------------------------------------------------

4. Stool examination -----------------------------------------------------------------------------

5. Syphilis test -------------------------------------------------------------------------------------

6. T.B Test ---------------------------------------------------------------------------------------

7. Ear Test ---------------------------------------------------------------------------------------

8. Eye Test ---------------------------------------------------------------------------------------

9. Spleen Test ---------------------------------------------------------------------------------------------

10. Abdomen Test-----------------------------------------------------------------------------------

11. Additional information or any other physical, mental, hereditary or intoxication diseases.

---------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------

(Please state nature of treatment)

...................................................................................................................................

I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ not to pursue further education.

Signature --------------------------------------------
Designation ------------------------------------------
Station ----------------------------------------------
Date: --------------------------------------------------------------
Official stamp ------------------------------------------------ -------------------------------